

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na: 025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA
MAPOKEZI YA SHILINGI BILIONI 3.8 ZA UKAMILISHAJI WA HOSPITALI YA
MANISPAA YA SUMBAWANGA, UJENZI WA KITUO CHA AFYA, UKAMILISHAJI WA
ZAHANATI NA UNUNUZI WA VIFAA TIBA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inatoa taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha shilingi 3,820,000,000/= kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga, ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Senga, Manispaa ya Sumbawanga, ukamilishaji wa Zahanati katika Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Kalambo na Nkasi na ununuzi wa vifaa tiba vya vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Kalambo na Nkasi.

Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi 1,070,000,000/= zitatumika kwa ajili ukamilishaji wa majengo ya Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga, kiasi cha shilingi Milioni 500 kitatumika kwa ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Afya cha Kata ya Senga Manispaa ya Sumbawanga. Kiasi cha milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati moja Manispaa ya Sumbawanga.

Aidha kiasi cha shilingi Milioni 100 kimepokelewa kwa ajili ya kufanya ukamilishaji wa Zahanati mbili katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Halmashauri ya Kalambo imepokea kiasi cha shilingi Milioni 400 kufanya ukamilishaji wa Zahanati nane. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imepokea shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati nne. Kiasi cha shilingi 1,500,000,000 kimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Kalambo na Nkasi.

Mapokezi ya fedha hizo yataboresha huduma za afya katika Mkoa wa Rukwa. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kwa niaba ya wakazi wote inaendelea kuishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kuwezesha miradi ya maendeleo na kuboresha huduma za afya.

Imetolewa na

Khadija Dalasia
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Mkoa wa Rukwa
04 Oktoba 2023

